JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

MKUU WA TAKUKURU (M)
BARABARA YA BOMBO HOSPITALI
S.L.P. 1953,
Simu Nambari: 027-2645186,
Nukushi: 027-2647885
Barua Pepe: *rbctanga@pccb.go.tz*
Wavuti: www.pccb.go.tz
21105 TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU MKOA WA TANGA YAFANIKIWA KUREJESHA SHILINGI 173,120,570/= ZA SERIKALI NA WANANCHI.

Ndugu wanahabari,

Habari za asubuhi,

Nimewaita hapa leo tarehe 09/07/2020 ili nizungumze na wananchi wa Mkoa wa Tanga na Tanzania kwa ujumla kupitia ninyi Waandishi wa Habari kwa lengo la kuujulisha umma juu ya utekelezaji wa majukumu ya Taasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa Mkoa wa Tanga kwa kipindi cha Aprili – Juni 2020.

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii ya kipekee ya kukutana nanyi siku ya leo katika Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Kilindi, karibuni sana.

Kwa Ujumla na kwa Ufupi nitazungumzia kazi zilizofanywa na TAKUKURU Mkoa wa Tanga katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2020 na pia mikakati yetu kuelekea Uchaguzi Mkuu unaokuja wa Rais, Wabunge na Madiwani tukio ambalo limepangwa kufanyika Oktoba, 2020.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Tanga, imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kuratibu na kuongoza mapambano dhidi ya Rushwa kwa kuchukua hatua zinazofaa kwa lengo la Kuzuia na Kupambana na vitendo vya rushwa katika idara za Serikali, mashirika ya umma na Taasisi binafsi mkoani Tanga kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007 (pamoja na kanuni zake za mwaka 2009). Majukumu haya tumekuwa tukiyatekeleza kwa kushirikiana na ofisi zote za TAKUKURU Wilaya zilizopo kwenye Mkoa wa Tanga pamoja na wananchi kwa ujumla, ambapo kwa robo ya Aprili hadi Juni 2020 tumetekeleza mambo mengi na hii ni taarifa ya baadhi ya tuliyoyatekeleza:

1) TAKUKURU YAMRUDISHIA MWANANCHI KIWANJA ALICHOPORWA NA MWENYEKITI WA KITONGOJI MIAKA MINANE ILIYOPITA

Ndugu wanahabari,

Mnamo tarehe 21/04/2020 Ofisi za TAKUKURU Wilaya ya Pangani ilipokea taarifa ya malalamiko toka kwa Bi Cheusi Mosha Njere akimlalamikia Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kumba katika kijiji cha Pangani Magharibi Oscar Albert Mbuguni kuwa anatumia madaraka yake vibaya na kumdhulumu kiwanja chake namba 24 kitalu H Miono na kumpatia mke wake.

Ilielezwa kwamba awali kabla ya zoezi la upimaji wa viwanja, mlalamikaji alikuwa na eneo lake alilokuwa anamiliki kwa njia za kimila. Kwamba zoezi la upimaji lilifanyika kati ya Mwaka 2011 na 2012 eneo lake hilo lilitoa viwanja vitano (05) ambapo yeye mwenyewe alipewa viwanja vitatu ambavyo ni viwanja namba 20, 21 na 22, kiwanja namba 23 alipewa mtu

mwingine aitwaye Mohamedi na kiwanja kingine namba 24 kitalu 'H' Miono/ Mwembekodi kilibaki wazi huku Mwenyekiti huyo akidai kuwa kiwanja hicho kuna mtu ameuziwa na watu wa Idara ya Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani.

Kwamba tangu kipindi hicho hakuna mtu yoyote aliyejitokeza kuwa ni mmiliki wa kiwanja hicho hadi pale Mwenyekiti huyo akiwa na nia ovu ya kukitwaa kiwanja hicho alipotuma watu wa kufanya usafi na mlalamikaji alipomuuliza, mwenyekiti huyo alijibu kuwa kiwanja hicho ni mali yake huku akimwambia mlalamikaji kuwa mwanamke hastahili kumiliki viwanja vingi.

Ndugu wanahabari,

Baada ya kupokea malalamiko hayo TAKUKURU Wilaya ya Pangani ilifanya uchunguzi na ikabainika kwamba mwenyekiti huyo hakuwa na kiwanja katika eneo hilo bali alikuwa anatumia madaraka yake vibaya kutaka kujinufaisha. Aidha mwenyekiti huyo alipohojiwa na TAKUKURU alikiri kuwa ni kweli kiwanja hicho ni mali halali ya mlalamkaji na kwa hiyari yake mnamo tarehe 05/05/2020 aliandika hati ya kukabidhi kiwanja hicho na kumwandikia Bi Cheusi Mosha Njere barua ya kwenda kulipia na kumilikishwa kiwanja chake.

2) TAKUKURU YAKAMATA DAWA ZINAZOUZWA NA WATUMISHI WA AFYA KWENYE DUKA LA DAWA LA HOSPTALI YA WILAYA YA PANGANI

Ndugu wanahabari,

Mnamo tarehe 20/05/2020 TAKUKURU Wilaya ya Pangani ilipokea taarifa za kiintelejensia kuwa kuna watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Pangani kitengo cha BIMA wanatumia Dirisha la Dawa la wateja wa BIMA kuuza dawa zao binafsi badala ya zile za Serikali.

Kwamba watumishi hao wamekuwa wakinunua dawa kinyume na utaratibu unaotakiwa na kuziingiza kwenye duka hilo na kuziuza kwa wagonjwa na hawatoi risiti. Taarifa hiyo ilieleza kuwa Medical Officer Incharge wa Hospitali hiyo akishirikiana na Muuguzi aitwaye Augustino Norasco wamekuwa wakitumia fedha zinazotokana na mauzo ya dawa kwenye dirisha hilo kwa maslahi yao binafsi.

Ndugu wanahabari,

Baada ya kupokelewa taarifa hii uchunguzi wa awali ulianzishwa na mnamo tarehe 21/05/2020 majira ya saa mbili usiku maafisa wa TAKUKURU walifanya operation katika hospitali hiyo ya Pangani na kufanikiwa kukamata shehena ya dawa box mbili (02) zilizonunuliwa na wahusika na kuziingiza kwenye duka hilo la bima kwa lengo la kuziuza kwa maslahi yao.

Uchunguzi umebaini kuwa dawa hizo zilinunuliwa toka duka la MD Pharmacy lilipo jijini Tanga kwa thamani ya Shilingi 340,500/=. Aidha imebainika kuwa watuhumiwa hao walianzisha duka hewa na kulipa jina la *PANGANI MEDICS* na kulitumia kununulia dawa na kuziuza kupitia duka la hospitali ya Wilaya ya Pangani kinyume na Sheria, taratibu na miongozo inazosimamia uagizaji na utumiaji wa dawa kwenye Hospitali za Serikali. Kwa sasa dawa zimekabidhiwa kwa Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO) ili azihifadhi na utaratibu wa kuziteketeza (disposal) unaendelea.

3) TAKUKURU YAFANIKISHA UREJESHWAJI WA Shilingi 4,218,570.00 KWENYE AKAUNTI YA DED MUHEZA

Ndugu wanahabari

TAKUKURU Wilaya ya Muheza, ilipokea taarifa kwa njia za kiintelejensia, iliyobainisha kuwa baadhi ya watendaji wamekuwa wakitumiafedha za makusanyo yanayotokana na ushuru wa Halmashauri kwa njia ya POS kwa maslahi yao jambo lililopelekea Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kukosa mapato yake.

Uchunguzi ulianzishwa na kubaini tuhuma kuwa ni kweli na hivyo TAKUKURU iliwataka warejeshe fedha hizo, kati ya wadaiwa hao mmoja anayefahamika kwa majina ya EDMUND ZONGWE, Afisa Mtendaji wa kata ya Ngomeni tarehe 23 Machi, 2020 ameweza kurejesha

kiasi cha Shilingi 4,218,570.00 kwenye akaunti namba 41910000340 ya DED MUHEZA kati ya Shilingi 14 Milioni anazodaiwa. TAKUKURU inafuatilia kwa karibu urejeshwaji wa fedha hizo

4) TAKUKURU YAFANIKISHA UDHIBITI WA Shilingi 3,515,000/= Milioni KWA UMOJA WA CHAMA CHA WAFUGAJI WA NG'OMBE WA MAZIWA MLINGANO (UWAMLI)

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Wilaya ya Muheza Ilipokea taarifa kuwa viongozi wa awamu iliyopita wa chama tajwa, wamefanya ubadhirifu wa lita elfu 21 za maziwa zenye thamani ya Shilingi 15Milioni kwa maslai yao binafsi. Jambo lililopelekea umoja huo kushindwa kujiendesha na pia baadhi ya wafugaji kukosa stahiki zao. Baada ya kupata taarifa hiyo uchunguzi ulianzishwa na kubaini tuhuma ni ya kweli na kwamba viongozi waliohusika na ufujaji huo wametakiwa kurejesha fedha hizo kabla au ifikapo tarehe 31 Julai 2020.

Tarehe 30 Juni walianza kurejesha kiasi cha Shilingi 3,515,000/= (taslimu) ambazo zimehifadhiwa kwenye akaunti ya ofisi ya TAKUKURU (W) Muheza na baada ya kiasi chote kukamilika tunatarajia kukabidhi fedha hizo kwa uongozi wa chama hicho.

5) TAKUKURU YAFANIKISHA UREJESHWAJI WA FEDHA Shilingi 320,000/=KWA UONGOZI WA KIJIJI CHA BWITINI.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Wilaya ya Muheza Ilipokelewa taarifa kuwa aliyekuwa Kaimu Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Bwitini amefanya ubadhirifu wa Shilingi 320,000/= fedha ambazo zilikuwa ni michango ya wananchi kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya kata ya Mhamba. Kutokana na hilo, baada ya wananchi kufahamu kuwa fedha zao zimefujwa walikataa kuendelea kuchangia ujenzi wa kituo hicho cha Afya.

Uchunguzi ulianzishwa na kubaini tuhuma ni ya kweli na baada ya kukamilika mtuhumiwa aliamua kukabidhi fedha hizo ambazo alikaa nazo kwa takribani miezi 22

bila ya kuwasilisha kwa uongozi wa kata ambao ndiyo unasimamia ujenzi. Tarehe 05/02/2020 mtuhumiwa alirejesha fedha hizo (taslimu) kwa uongozi wa Kijiji cha Bwitini kupitia stakabadhi namba 417761 na 417762 zote za tarehe 05/02/2020.

6) TAKUKURU YAOKOA FEDHA ZA WANANCHI SHILINGI 1,591,000.00 MILIONI KATIKA KATA YA KERENGE

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Wilaya ya Korogwe ilipokea taarifa kuhusu ubadhirifu wa fedha zilizochangwa na wananchi wa vijiji vinne (4) vya kata ya Kerenge kwa ajili ya kusafisha eneo ilipotakiwa kujengwa hospitali ya wilaya Korogwe. Uchunguzi ulibaini kuwa, kila kaya katika kata hiyo ilipaswa kuchanga Shilingi 2,000.00 (elfu mbili) na katika kaya zilizochanga jumla ya fedha zote zilizopatikana ni Shilingi 2,597,000.00 ambapo wahusika Wakuu wa kukusanya michango hiyo walikuwa ni Maafisa Watendaji wa Vijiji.

Vijiji hivyo vilivyotakiwa kuchanga na jumla ya fedha zilizochangwa ni kama ifuatavyo: Kijiji cha Kibaoni kilichanga Shilingi 1,148,000.00, Makaburini Shilingi 410,000.00, Vingo Shilingi 386,000.00 na Mapangoni Shilingi 653,000.00.

Aidha, mpaka uchunguzi unafanyika ni kiasi cha Shilingi 1,006,000.00 tu ndicho ambacho kilikuwa kimewasilishwa ofisi ya kata kwa ajili ya matumizi ya kusafisha eneo la kujenga hospitali ya Wilaya kama ilivyokusudiwa kati ya Shilingi 2,597,000.00 zilizokusanywa kutoka kwa wananchi, Hivyo kufanya jumla ya Shilingi 1,591,000.00 kutowasilishwa katika akaunti ya kata tangu mwaka 2019 zilipokusanywa.

Ndugu wanahabari,

Uchunguzi ulibaini kwamba, kati ya fedha hizo, Afisa Mtendaji wa kijiji cha Kibaoni aliwasilisha Shilingi 300,000.00, Makaburini Shilingi 225,000.00, Vingo Shilingi 200,000.00 na Mapangoni Shilingi 281,000.00. TAKUKURU baada ya kubaini ubadhirifu huo, uliwaagiza maafisa watendaji hao kurejesha fedha walizobaki nazo katika akaunti ya kata na ndipo jumla ya Shilingi 1,591,000.00 zilirejeshwa kwenye akaunti ya kata

yenye namba 415100225441 iliyopo katika benki ya NMB ili zikafanye kazi ya kusafisha eneo ambalo kwa sasa kinajengwa kituo cha Afya Kerenge.

Kwa kifupi:

Na.	Jina la Kijiji	Fedha Zilizokusanywa Shilingi	Fedha Zilizowasilishwa Awali Shilingi	Fedha Zilizookolewa Shilingi
1	KIBAONI	1,148,000.00	300,000.00	848,000.00
2	MAKABURINI	410,000.00	225,000.00	185,000.00
3	VINGO	386,000.00	200,000.00	186,000.00
4	MAPANGONI	653,000.00	281,000.00	372,000.00
5	JUMLA	2,597,000.00	1,006,000.00	1,591,000.00

Mbali na utekelezaji wa kazi hizo TAKUKURU Mkoa wa Tanga katika kipindi hicho cha Aprili hadi Juni, 2020 pia ilifanya kazi katika maeneo ya Uchunguzi na Mashitaka, Udhibiti wa Mianya ya Rushwa pamoja na Elimu kwa Umma kama ifuatavyo:

7) UCHUNGUZI NA MASHITAKA.

Ndugu wanahabari,

Katika Uchunguzi, TAKUKURU Mkoa wa Tanga tumepokea jumla ya taarifa **113** za vitendo vya Rushwa kwa kipindi cha Aprili hadi Juni 2020. Mchanganuao wa taarifa hizo kiidara inaonyesha kwamba Halmashauri za Serikali za vijiji **28,** Ardhi **13**, Misitu 1, Fedha 1, Mahakama **6**, Elimu **9** na Biashara **4**, Idara zingine ni Siasa **13** na Jeshi la Polisi **6**, Vyama vya ushirika **6**, Sekta binafsi **2**, Mashirika ya Hifadhi ya Jamii **3**, Mifugo **1, Viwanda 2,** na Maji **2.** Aidha, uchunguzi wa taarifa **86** unaendelea katika hatua mbalimbali, taarifa **19** zilifungwa baada ya watoa taarifa kushauriwa hatua stahiki za kuchukua kufuatia kubainika kwamba taarifa hizo si za vitendo vya rushwa na taarifa **08** zilihamishiwa idara zingine kwa hatua mbalimbali za kisheria.

Kwa upande wa uendeshaji mashitaka TAKUKURU Mkoa wa Tanga kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi June 2020, imeendesha jumla mashauri **19** mahakamani ambapo mashauri yote yalifunguliwa kabla ya Aprili 2020 na hakuna shauri lililofunguliwa kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2020.

Aidha kati ya kesi hizo **19** zilizoendeshwa mahakamani kesi **2** zilitolewa hukumu katika Mahakama za wilaya za Handeni na Muheza ambapo watuhumiwa waliachiwa huru baada ya kutokutwa na hatia kwa makosa waliyokuwa wakituhumiwa kuyafanya kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na rushwa namba 11/2007.

Aidha katika kesi 1 ambayo ni CC 110/2017 iliyokuwa ikiendeshwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Tanga, Mtuhumiwa ZAINABU ABDILAHI FADHILI alipatikana na Hatia ambapo alihukumiwa kwenda jela miaka 3 na kurejesha fedha kiasi cha **Shilingi 5,500,000.00** (Shilingi milioni tano na laki tano) za Serikali ambazo aliiba kinyume na Sheria.

8) UZUIAJI RUSHWA:

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Tanga, Kupitia Dawati la Uzuiaji Rushwa, kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni, 2020 imeendelea kufanya kazi mbalimbali zinazolenga kudhibiti mianya ya rushwa katika sekta mbalimbali. Miongoni mwa kazi zilizofanyika ni pamoja na kazi ya Uchambuzi wa mifumo 7 katika maeneo mbalimbali ambayo ni Halmashauri, Vyama vya Ushirika na Uhifadhi wa wanyama pori. Chambuzi hizo za mifumo zilifuatiwa na warsha/ vikao 2 pamoja na kazi 4 za Ufuatiliaji wa maazimio yanayotokana na warsha mbalimbali zilizofanyika katika kipindi tajwa.

9) UFUATLIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO:

Katika utekelezaji wa majukumu yake kupitia Dawati la Uzuiaji Rushwa, kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni, 2020 TAKUKURU (M) Tanga imefanya ufuatiliaji wa miradi **16** ya maendeleo katika Wilaya mbalimbali za Mkoa wa Tanga yenye thamani ya Jumla ya Shilingi

Bilioni tatu, milioni mia moja kumi na saba na arobaini na tano elfu, mia saba na mbili na senti hamsini tu. (**Shilingi 3,117,045,702.50**).

Kazi ya ufuatiliaji wa miradi hiyo inaendelea kufanyika kwani baadhi ya miradi haijakamilika na baadhi inaonekana kuwa na kasoro. Aidha miradi iliyofuatiliwa ni katika sekta za Elimu, Afya, Maji na barabara. TAKUKURU (M) Tanga, tumefuatilia matumizi ya fedha **za Serikali zinazotengwa kwa matumizi mbalimbali katika ofisi za serikali na taasisi za umma.**

Ufuatiliaji huu hufanyika kwa kufuatilia mtiririko wa fedha kutoka chanzo (Hazina, Wafadhili au Vyanzo vya ndani) mpaka mahali fedha zilipolengwa kutumika. Moja ya maeneo ambayo ufuatiliaji umefanyika ni matumizi ya fedha za chakula cha wanafunzi katika shule maalum za msingi za kutwa na bweni (capitation grants) Mkoani Tanga.

FEDHA ZILIZOOKOLEWA KUTOKANA NA KAZI ZA UCHUNGUZI NA UDHIBITI.

Katika utekelezaji wa majukumu yake ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU Mkoa wa Tanga katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2020 imepata mafanikio ya kuokoa/ kudhibiti fedha kutokana na kazi za uchunguzi na udhibiti.

Kwa Uchache, Mafanikio na matokeo ya moja kwa moja yaliyopatikana ni pamoja na haya yafuatayo: TAKUKURU Wilaya ya Muheza kusaidia urejeshwaji wa fedha **Shilingi 8,359,000/=** za wananchi watatu baada ya Matarajio yao ya kupata viwanja kwa ajili ya biashara kushindikana. TAKUKURU Wilaya Kilindi imefanikiwa kuokoa fedha **Shilingi 4,656,000/=** katika mradi wa maji Kwediboma na kiasi cha **Shilingi 1,188,000/=** zimeokolewa katika miradi ya ujenzi wa madarasa katika shule tano tofauti Wilayani Kilindi.

Vile vile TAKUKURU Wilaya ya Handeni imeokoa kiasi cha **Shilingi 2,150,000/**= pesa za Halmashauri ya Wilaya ya Handeni zilizokuwa zimekopeshwa Saccoss mbalimbali kati ya mwaka 2012 na 2013. Aidha TAKUKURU Wilaya ya Lushoto, imefanya udhibiti wa fedha kiasi cha **Shilingi 133,500,000/=** ambazo zilikuwa zikusanywe na Shule ya Sekondari Mazinde Juu kutoka kwa wazazi/walezi wa wanafunzi wa kidato cha sita kama malipo ya ziada kinyume na Sheria pamoja na kiasi cha **Shilingi 6,800,000/=** ambazo zilikuwa

zilipwe shule ya Sekondari ya Kifungilo na wazazi/walezi wa wanafunzi wa kidato cha sita kwa madai ya kununua matunda kwa ajili ya wanafunzi kujikinga na corona.

TAKUKURU Wilaya ya Pangani pia imefanikiwa kuokoa **Shilingi 3,470,000/=** za Serikali ambazo hazikuwasilishwa na Afisa Biashara wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani baada ya kufanya mauzo ya Vitambulisho 174 vya wajasiriamali. Afisa huyo alirudisha fedha hizo mwezi Juni 2020, **Shilingi 620,000/=** za Serikali ya Kijiji cha Mtango zilizokuwa zifanyiwe ubadhilifu kutokana na Serikali ya kijiji kutoweka wazi fedha zilizotolewa na mfadhili kwa maendeleo ya kijiji zilirudishwa mwezi Mei na Juni mwaka 2020. Pia **Shilingi 1,150,000/=** za SACCOS ya UVIPASA ambazo zilikopwa bila kurejeshwa tangu mwaka 2014 zilirudishwa na wakopaji, mwezi Juni mwaka huu 2020.

Hivyo Kwa Upande wa fedha zilizookolewa/ kudhibitiwa kutokana na kazi za uchunguzi na udhibiti, Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Tanga Katika kuzuia na kupambana na rushwa, tumefanikiwa kuokoa fedha taslimu kiasi cha **Shilingi 173,120,570,00** zilizotokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa dhidi ya miamala mbalimbali ambayo haikuwa rafiki kwa Sheria, taratibu na kanuni mbalimbali.

10) ELIMU KWA UMMA

Ndugu wanahabari,

Kwa upande wa jukumu la Kuelimisha Umma, kwa mujibu wa kifungu cha 7(b) cha sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007, TAKUKURU inalo jukumu la kuhimiza na kuendeleza uungaji mkono wa jamii katika kupambana na vitendo vya rushwa. Jukumu hili hutekelezwa kupitia Dawati la Elimu kwa Umma.

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Tanga tumeelimisha umma kwa kuendesha semina 8, mikutano ya hadhara 14, Ufunguzi wa Klabu mpya 08 za wapinga rushwa na Uimarishaji klabu 27 za wapinga rushwa zilizopo katika shule na Taasisi mbalimbali Mkoani Tanga, sambamba na kuandaa Habari na Makala 05. TAKUKURU Mkoa wa Tanga pia tumefanya vipindi vya redio 22 kupitia vituo vya redio vilivyopo mkoani Tanga na tulitoa taarifa nne (4) kwa umma kupitia vyombo vya habari vilivyopo Mkoani hapa.

Napenda nitumie fursa hii kuwashukuru walimiki wa vyombo hivyo pamoja na wafanyakazi wao wote kwa kuwa sehemu ya kufanikisha hilo kwani mmekuwa mkiitika wito kila tulipo waita, Ahsanteni sana. TAKUKURU Mkoa wa Tanga Tunahamasisha na kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa tukiamini kwamba wananchi wakiwa na uelewa kuhusu rushwa watachukua hatua ya kutoa taarifa, kukemea na kushirikiana na Serikali kwa hali na mali katika mapambano haya dhidi ya adui Rushwa.

11) HITIMISHO

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Tanga katika kipindi cha mwaka mpya wa fedha (mwezi Julai hadi Septemba mwaka 2020) ambacho pia ni kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, mikakati yetu tuliyonayo ni pamoja na:

i. Kuendelea kufanya uchunguzi wa malalamiko ya vitendo vya rushwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya rushwa ili kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria kutegemeana na ushahidi unaopatikana.

ii. Kuendelea kufanya udhibiti kwa kuchambua mifumo mbalimbali ili kubaini mianya ya rushwa na kushauri jinsi ya kuziba mianya hiyo kwa lengo au nia ya kudhiti rushwa kwenye mifumo husika.

iii. kuendelea kutoa elimu na kuwahamasisha wananchi, watangazania na wagombea waache kujihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa iwe kwenye mifano ya zawadi, shukrani au jina lolote lile na iwe ni fedha taslim, kanga, vitenge au kitu chochote kile. Tunawaomba wananchi wasikubali kuuza utu wao kwa kupokea rushwa itakayowapelekea kupata viongozi wasio waadilifu jambo ambalo litawagharimu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Tunawaomba waongeze ushiriki wao katika mapambano haya dhidi ya Rushwa kwa kufichua vitendo vyote vinavyoashiria uwepo wa Rushwa hasa wakati huu wa maandalizi ya uchaguzi Mkuu.

Aidha TAKUKURU tutahakikisha tunafuatilia matukio yote yanayohusu vitendo vya Rushwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi na kuchukuliwa hatua stahiki kwa wahusika wa vitendo hivyo bila huruma wala upendeleo. TAKUKURU Mkoa wa Tanga tutaendelea pia na kazi ya kufatilia urejeshwaji wa fedha za madeni ya vyama vya ushirika na pia miradi ya maendeleo ili maendeleo ya kweli ya wananchi yaliyokusudiwa na Serikali yetu yaweze kupatikana.

Ni jukumu la kila Mtanzania kuendelea kushirikiana na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya Rushwa pasipo kuoneana aibu kwani athari ya rushwa ni ya taifa zima.

TAKUKURU Mkoa wa Tanga inaendelea kutoa wito na kuwakaribisha wananchi na wadau wote wa Mapambano dhidi ya Rushwa kufika ofisi zetu kutoa taarifa kwa njia yoyote watakayo ona mwafaka kwao. Mwananchi au mdau yeyote anaweza kuwasiliana moja kwa moja na viongozi wa TAKUKURU Mkoa wa Tanga ni kwa namba zifuatazo:-

- 0689-797-998 na 0738-150-225(Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tanga)
- 0784-280-663 na 0738-150-228 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Kilindi)
- 0782-208-008 na 0738-150-232 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Muheza)
- 0784-743-303 na 0738-150-230 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Lushoto)
- 0786-207-311 na 0738-150-233 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Pangani)
- 0718-666-656 na 0738-150-231 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Mkinga)
- 0784-428-183 na 0738-150-229 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Korogwe)
- 0688-313-853 na 0738-150-227 (Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Handeni)

Pia mtoa taarifa aneweza kupiga simu ya Bure 113 au ukatuma ujumbe mfupi wa maandishi kwa kupiga *113# na kufuata maelekezo.

Dkt. Sharifa O. Bungala
KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M)
TANGA
Imetolewa TAKUKURU WILAYA YA KILINDI Juni 09, 2020